



equinor

## Sera ya Haki za Binadamu

### Mkakati wetu

Tutafanya shughuli zetu kulingana na Kanuni za Mwongozo wa Umoja wa Mataifa (UN) kuhusu Biashara na Haki za Binadamu na kanuni kuni za Athari ya Kimataifa ya Umoja wa Ulaya. Tunaheshimu haki zote za binadamu zinazotambuliwa kimataifa, ikiwemo zile zilizowekwa katika Sheria ya Kimataifa kuhusu Haki za Binadamu na Tamko la Shirika la Wafanyakazi Kimataifa kuhusu Kanuni na Haki Msingi Kazini. Hii ni pamoja na lakini si tu haki ya binadamu ya uhuru wa kuwa kwenye chaba na makubaliano ya Pamoja na haki za binadamu zisihusu ajira ya kulazimishwa, ajira kwa watoto au ubaguzi kuhusiana na ajira na taaluma. Pia tunaheshimu viwango vinavyotumika vya sheria ya kibinadamu ya kimataifa.

Sera hii inabainisha kanuni za jinsi tunavyohusiana na waajiriwa wetu, wakandarasi, wagawaji na wabia wetu na pia jamii zilizoathirwa na shughuli zetu za biashara. Tutaepuka kukiuka haki za binadamu wengine na kujitahidi kuangazia ipasavyo athari mbaya za haki za binadamu tunazohusika. Tutaangazia haswa haki za binadamu ambazo tunaweza tuka katika hatari ya kuathiri watu wengi na watu welio kwenye hatari kubwa ya athari mbaya, wakiwemo wanawake, watoto, wafanyakazi wahamiaji na watu wa asili.

Kwa kutumaini kuwa utendakazi wetu utakua tunapimarisha desturi zetu, tutaendelea kujitahidi kuboresha jitihada zetu za haki za binadamu.

### Tunaahidi

Kuheshimu haki zote za binadamu zinazotambuliwa kimataifa, kwa mujibu wa Kanuni za Mwongozo wa Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Biashara na Binadamu na haswa;

- Kuwatendea haki wale wanaofanya kazi nasi na wale wanaoathiriwa na shughuli zetu na bila ubaguzi
- Kudumisha usalama na afya bora katika mazingira ya kufanyia kazi
- Kupinga aina zote za ulanguzi wa watu, ajira ya kulazimisha na aina haramu za ajira kwa watoto katika msururu wetu wa maadili
- Kuheshimu haki za watu katika jamii zilizoathiriwa na shughuli zetu ikiwemo, lakini si tu, haki ya mali, kazi na matumizi ya ardhi na maliasili, usalama, afya na haki ya maji na usafi
- Kufanya shughuli zetu kulingana na ahadi yetu ya kutii Kanuni za Hiari kuhusu Haki za Usalama na Binadamu

### Jinsi tunavyofanya kazi

- Tunawahitaji waajiriwa wetu wote na wakandarasi waliopewa ajira kutii sera hii na tutajenga uwezo kufikia kiwango hiki
- Tunatarajia wagawaji wetu na wabia wa biashara kufuata nia na kusudi la sera hii na kushiriki ahadi yetu ya kuheshimu haki zote za binadamu zinazotambuliwa kimataifa, ikiwemo zile haswa zilizorejelewa hapo juu, wakati wa kutufanyia au kufanya kazi pamoja nasi
- Tunatarajia wagawaji wetu wote na wabia wa biashara kuangazia haswa haki za binadamu ambazo wanaweza kuathiri sana na haki za watu walio kwenye hatari kubwa ya athari mbaya, ikiwemo wanawake, watoto, wafanyakazi wahamiaji na watu wa asili
- Tunatarajia wabia wetu wa biashara ya uchimbaji na kawi kuahidi kutekeleza Kanuni za Hiari kuhusu Haki za Usalama na Binadamu
- Tutajizatiti kuonyesha ushawishi katika mahusiano yetu ya biashara ili kuepuka au kupunguza athari mbaya kwenye haki za binadamu zinazohusiana na shughuli zetu moja kwa moja
- Tutaendelea kutekeleza taratibu uchunguzi wa kutosha wa haki za binadamu wa jinsi tunavyofanya kazi iwezekanavyo

- Tutatathmini athari kamili na zinazoweza kutokea za haki za binadamu kutokana na shughuli na mahusiano ya biashara zetu, ikiwemo inavyofaa kwa ushirikiano kwa wakati na muhimu na wanajamii wa karibu wanaoweza kuathiriwa au walioathiriwa na kukusudia kutekeleza hatua za kuzuia na kupunguza vizuri zinapohitajika
- Tutatoa au kushirikiana, ikiwemo na wagawaji na wabia wetu wa biashara kutoa suluhisho linalofaa kwa watu binafsi, wafanyakazi na jamii za karibu, pale ambapo tumesababisha au tumechangia haki mbaya za binadamu. Kutokana na hayo, pia tutatoa au kushirikiana katika mbinu bora za manung'uniko inapohitajika
- Hatutazuia wadau walioathiriwa kufikia masuluhisho au njia nyingine za maluluhisho
- Pale ambapo sheria au mahitaji yanatuzuia kutumia sera hii, tutatafuta njia za kuhakikisha kuwa tunaheshimu haki za binadamu kwa kiwango kikubwa kinachowezekana
- Tutatathmini na kuripoti kuhusu maendeleo na utendakazi wetu